Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners,* pages 8-9.

**UTANGULIZI**

Katika miongo mbili zilizopita ulimwengu umeona mwanzo mpya katika eneo la haki za kibinadamu ambapo umuhimu wa sheria za kimataifa na pia mafikira ya wananchi imetambulika. Kwa upande wa sheria za kimataifa, mbinu mpya zimegeuza mafikira yetu na vile ambavyo kutekeleza haki .Vile vile, mafikira mapya na ule moyo wa watu binafsi na vikundi kuleta mageuzi umegeuza mafikira yetu kuhusu yale ambayo twaweza kufanya kwa uwanja wa haki za kibinadamu- na kwa hivyo yale ambayo twaweza kutimiza.

Kote duniani, mashambani na serikalini na pia kwenye maeneo makuu ya sheria za kimataifa, watu wanaunda na kutumia, mbinu na njia mbali mbali za kuhakikisha kwamba kazi yao yatekelezwa vyema. Mradi wa Mbinu Mpya Kwa Haki Za Kibinadamu (*New Tactics in Human Rights Project*) umezichukua hizi mbinu mpya na kuzisambaza kwa wengine ambao wanafanya kazi kwa uwanja wa haki za kibinadamu. Mwakaribishwa nyote kushangilia hii kazi na kutumia hiki kitabu kilicho mikononi mwenyu kama chombo maalum.

Nikifikiria kazi yangu ambayo nafanya, naona fursa mpya ya kuwapa haki wale ambao haki zao zimekiuka. Kuanzishwa kwa koti ya jinai ya iliyokuwa Yugoslavia na Rwanda, ambayo iliyokuwa koti ya kwanza ya jinai za vita imeleta mafikira mapya kwenye mataifa na pia zilifungua milango mipya za haki. Wajuzi waliuotumika kwenye hizo koti kutoka nchi mbali mbali walitenda kile ambacho hakijatendwa awali- kuunda sheria mpya na kuanzisha desturi mpya kwa kushtaki washtakiwa na mashtaka ambayo yalikuwa hayajatumika na nchi yeyote ulimwenguni. Hayo yote yalizaa mbinu mpya ambazo zilifungua njia ya mbinu kuu- Koti ya Jinai ya Kimataifa ( *International Criminal Court).* Koti hii sasa yatupatia chombo cha kulinda na kutekeleza haki bila kujali ni wapi ama ni nani aliye kiuka hizo haki za kibinadamu.

Mbinu mpya pia ilitumika zile nyakati za koti ya jinai ya iliyokua Yugoslavia kwa kushtaki waliokuwa polisi wa Bosnia na mashtaka ya Kunajisi wanawake waislamu wa Bosnia. Hii mbinu imewezesha sheria na haki kutekelezwa mara mingi.

Miaka kumi iliyopita, wanasheria wangepumbaza swala la kumushtaki aliyekuwa Rais Agusto Pinochet. Wakati huo, wahalifu _walikuwa wanajidai wakizurura kote ulimwenguni bila pingamizi. Kushikwa na kushtakiwa kwa Pinochet kulibadilisha mafikira ya wanaopigania haki za kibinadamu.

Nashangilia harakati za wanaopigania haki za kibinadamu kutumia koti za kitaifa na za kimataifa kujulisha ulimwengu kesi za jinai popote ambazo zinatokea. Lakini haya ni chache tu kwa zile mbinu mpya zinazo tumika kupigania haki za kibinadamu popote ulimwenguni.

Najivunia kuungana na mradi wa mbinu mpya kwa haki za kibinadamu ( *New Tactics in Human Rights Project*) kwa kutoa hii maktaba. Na ingawa haiwezi kusemekana kuwa

kamilifu, hii ni maktaba iliyojaa mawazo mapya na mbinu mpya ambazo zaweza kusaidia yeyote kutekeleza kazi yake.

-Jaji Richard J. Goldstone

Jaji mstaaafu wa Koti ya Katiba ya Afrika Kusini
Mshtaki mkuu wa Koti ya Jinai ya iliyokuwa Yugoslavia na Rwanda
Mwenye kiti wa Koti ya Kimataifa ya Kosovo
Mwenyekiti wa Tume ya Kimataifa ya Kuchunguza Ujangili iliyoanzishwa na International Bar Association.

**UHAJI WA MBINU MPYA**
**NYENDO MPYA ZA HAKI ZA BINADAMU**

Miongo iliyopita imeiona mienendo mipya ya haki za binadamu ikifanikiwa kustawisha haki za binadamu na pia kutafuta njia ya kuzilinda. Mfano ni:

- Kulaani kuteswa
- Kulinda haki za wanawake na watoto
- Harakati halali za kisiasa
- Wafungwa wa kisiasa wamelindwa na kuachiliwa huru
- Kufuatilia kiada za haki za binadamu

Hatuwezi kuzidi kuhimiza umuhimu wa haya majilio au mapato na vile ilikuwa vigumu kuyatekeleza.

**Mbinu kwa nyendo za haki za binadamu**
Mbinu tatu zilichangia kwa haya maendeleo:

1. Kustawisha desturi za kimataifa ambazo ziliunda jamii ya kanuni, mapatano na kiada
2. Kuchunguza kutimizwa kwa kiada
3. Kulaani au kuaibisha vitendo vya serikali au kutotenda ikiwa kiada zakiukwa

**Upungufu**
Ni wazi kuwa hizi mbinuzimeleta maendeleo makuu na inapasa ziendelee kunusuriwa na kufwatiliwa. Ni wazi pia kuna malemeo makuu kwa yale twaweza kufanya kutumia hii njia na sio maridhawa kuchambua maswala makuu kutumia njia hii.

**Kueneza hii nyendo**
Inasemekana kuwa huu mradi wa kuendeleza haki za binadamu wahitaji kuunda uwanja pana ambao utachukua watu wengi kutoka sekta zote za umma.
Pia yahitaji kuendeleza mikakati kamilifu ambazo zaweza kutekelezwa kutumia mbinu tofauti tofauti ambazo zinatumuka.

**Mizuka ya mbinu mpya**
Kote ulimwenguni, wanaharakati wa haki za binadamu waliojitolea wameanzisha kazi hii:

- Kukuza mbinu mpya
- Kujenga mitandao isiyo tarajiwa
- Kujifunza kutoka kwa sekta zisizo tarajiwa

Mradi wa mbinu mpya wa haki za binadamu (*New Tactics for Human Rights Project*) una nia ya kuwaleta pamoja hawa wazushi na kutumainisha wengine na kazi yao. Zikiwekwa pamoja, hizi visa zawakilisha mizuka ya yale tunayoweza kutekeleza kwa upande wa haki za binadamu.

**Faida Ya Kufikiria Kimbinu**
Katika msomo huu, tuna tahsarisha sababu sita ambazo tunaamini zitasaidia kujenga nyendo sawa ya haki za binadamu:

1. Yale ambayo tunajua inaathiri yale tunaamini twaweza kufanya; mbinu zinasaidia kuamua mkakati
2. Mbinu tofauti yaambatana na shabaha tofauti
3. Mbinu tofauti zinavutia maeneo tofauti
4. Unyumbufu wa mbinu ni chanzo cha miujiza
5. Mbinu zafunza washiriki na wazhunguzi njinsi ya kujishughulisha ulimwenguni
6. Mbinu ni njia ya kufunza na kushughulisha washiriki na waandani kwenye kazi ya kikundi

**1. Mbinu zapenya njia mpya**

Yale ambayo twajua kufanya yathiri yale tunaamini twaweza kufanya; mbinu zasaidia kuchagua mkakati. Tukifikiria vile tutakavyofanya, twaweza kuzuia maoni yetu kwa yale ambayo twaweza kutekeleza. Historia imejaa na mifano ambayo jawabu moja inatumika mara kwa mara bila ushindi, au ambapo mbinu mpya inachukuwa mahala pa mbinu mzee.

**Mfano: Mbinu yaamua mkakati**

BAOBAB ya Haki za Akina Mama (BAOBAB) na (*Civil Resource and Documentation Centre-CIRDDOC)* kule Nigeria ilikuwa inapigania kujulisha umma juu ya uhasama dhidi ya wanawake. Watu wachache huko Nigeria waliamini kuwa wanawake wanastahimili uhasama. Serikali, polisi na hata vyombo vya habari havikutilia maanai swala hili.

Vyama visivyo vya serikali ( NGO) vilihabarishwa maathara ya tume ya Vienna na Tokyo na takabadhi ambazo zilivutia. Waliamua kujaribu mbinu mpya na walipanga tume duni ya uhasama dhidi ya wanawake. CIRDDOC ilitengeneza majaribio na tume duni kwenye jimbo la Amambra huko Nigeria ambayo ilikuwa inashughulikia swala la ukiukaji wa haki za binadamu. Tukio hili lilichukuliwa kama ushindi, kwa sababu watu wengi walihudhuria na ikasaidia kuleta majadiliano kwenye swala la kukiuka haki za binadamu kwa jumla na haki za akina mama. Mbinu ya kuunda tume duni ilileta matumaini.

Baadaye, Tume ya Taifa ya Nigeria Inayoshughulikia Uhasama Dhidi ya Wanawake (*Nigeria National Tribunal on Violence Against Women*) iliyoundwa ilivutia takabadhi ya wapasha habari na umma. Baada ya tume, hili swala lilisongelea kwenye ajenda ya umma na ikafungua njia timamu za kutumia mbinu tofauti kama kufundisha umma na mkandamizo. Tukio hili ni muhimu kwa pigano hili refu la kustawisha na kuhifadhi haki za akina mama kama haki za binadamu huko Nigeria.

**2. Mbinu Zaathiri Shabaha Vingine**

Mbinu tofauti zatumika vyeme kwa shabaha tofauti. Ni lazima tujifunze kuzimudu mbinu zetu kuambatana na shabaha zetu tukitafuta zile ambazo zitatupa matokeo kamili. Mbinu zikifeli kuathiri shabaha zetu, ni lazima tuunde mbinu mpya zitakazo tusaidia kufanya kazi.

**Mfano: Mbinu Zaathiri Shabaha Vingine**
Tume ya Haki za Kibinadamu na Uongofu Tekelezi (The Commission on Human Rights and Adminstrative Justice- CHRAJ) kule Ghana iliamua kushughulikia swala la Trokosi, mila inayotumika kwenye pande Fulani za nchi ambapo waganga wanaweka akina mama au wasichana kama watumwa ili kuomba msamaha kwa yale makosa au dhambi za jamaa zao.Hii tume ilitambua kuwa kutumia sheria kukomesha haya makosa haingefanikiwa na hata ingelazimisha hawa waganga kuendelea nah ii mila kisirisiri. Tume ilichagua kuzungumza na hawa waganga ikitumia njia tofauti. Ilitumia wazee wa kijiji na wataifa kwa majadiliano na wahalifu, wahanga, viongozi wengine wa umma na umma kwa jumla kuleta maelewano juu ya hiyo mila na pia ikipatiana abudi na njia za kuitupilia mbali hiyo mila bila kupoteza cheo. Kwa sababu walielewa shabaha yao, waliweza kuchagua mbinu zinazofaa. Wakati huu, zaidi ya wanawake na watoto 3,000 wameweza kuokolewa kutokana na mila ya Trokosi.

**3. Mbinu zajenga Maeneo**
Ikiwa jamii ya wanaopigania haki za kibinadamu yatumia mbinu moja au mbili tuu kushughulisha umaa itajikuta inavutia watu wachache tu ambao wanaelewa hiyo mbinu.Watu ambao wamezoea ubeberu wamejitenga na umma.Kuwashirikisha watu kama hawa, ni lazima tutumie mbinu zinazoambatana na mazoea au desturi zao.

**Mfano: Kujenga Maeneo**
*A mnesty Internationa (AI)* huko Netherlands ilionelea kuwa wale ambao walishiriki kwa mikakati yao ya Vitendo vya Dharura (Urgent Action) walikuwa wametimia miaka 30 na juu, lakini walitaka kuwasirikisha vijana pia. AI-Netherlands ilitumia maandishi kutumia teknologia ya simu ya mkono (Text Messaging Technology) kuwavutia na kushughulisha hawa vijana kwenye kampeni dhidhi ya kuteswa. Katika harakati za kuwafikia hili eneo, walisambaza kampeni zao kwenye tafrija za muziki na pia mahala pengine ambapo vijana hukusanyika.

**4. Unyumbufu wa Mbinu au Mikakati**
Unyumbufu wa mbinu ni chanzo cha miujiza.
Tukizidi kurudia zile mbinu ambazo tumetumia hapo awali, wapinzani wetu wanazoea hizo mbinu. Kumudu mbinu mpya zinasaidia kuweka wapinzani wetu macho.
Unyumbufu unakuza mafunzo kwenye pande zote.

**Mfano: Unyumbufu wa Mbinu**
Otpor! Chama cha wanafundi huko Serbia kilitumia mbinu flexibility kwenye harakati za kupigana dhidi ya utumwa kwenye milki ya Milosevic. Waliuita huu msogeo "Plan B." Serikali ya Serbia ilipoanza kuwashika waandamizi,Otpor! Ilipanga maandamano mengine kwenye stesheni za polisi ambapo waandamizi walioshikwa walikuwa wamewekwa. Hii ilipatia watu fursa ya kutupilia mbali uwoga wa kushiki kwenye maandamano. Pia ilisaidia kuvunja nguvu za milki ya Milosevic.

**5. Mbinu Zafunza Mashughuliko**

Mbinu zafunza washiriki jinsi ya kujishughulisha ulimwenguni. Tukiendelea kufanya mazoezi, mishipa yajifunza kusonga ikiupatia bongo fursa ya kupanga na kumudu njia mpya.Tukiendelea kufanya mazoezi, mambo yazidi kuwa rahisi.

**Mfano: Kufunza Washiriki Kujishughulisha Ulimwenguni**

Kote ulimwenguni, watu wanowekelea maanani mahala pa makumbusho ili kuafikiana na yale yaliyopita ili waweze kupanga yale yajayo. Kutoka kwa makumbusho ya kibinafsi, kufikia makumbusho kirasmi, Watu hukusanyika mahala za makumbusho wakitafuta uganguzi, maelewano na njia za kusonga mbele. Ukumbusho ni lugha muhimu ya wanaharakati wa kupigania haki za binadamu. Hapo ndipo ukiukaji wa haki za binadamu unaonekana na kujulikana, mambo hujadiliwa na mbinu za kuzuiza ukiukaji zakuzwa. Kwa ufupi hizi mahala zaweza kuwa chombo maalum cha kukuza desturi za haki za kibinadamu.
Muungano wa Kimataifa wa Mahala za Dhamira (International Coalition of Sites of Conscience) ni mtandao wa kimataifa wa mahala za kihistoria ambao unatumia nguvu za hizi mahala kufundisha umma jinsi ya kujishughulisha na mambo ya haki za binadamu. Kwa mfano, mshiriki mmoja Memoria Abieta anapanga kufungua Nyumba ya Ukumbusho kwenye jumba moja ambayo ilitumiwa kutesa watu ili wananchi "wakumbuke kuazima kusuluhisha matatizo ya nchi yetu."

**6: Mbinu ni Njia ya Kufundisha**
Mbinu ni njia ya kushughulisha washiriki na waandani kwenye kazi ya kikundi. Mbinu zingine zaweza kuwa za mda mfupi na zingine za mda mrefu. Lakini zote pamoja zahitaji mpango, uratibu na mwelekeo. Zinawapa wananchi fursa ya kushiriki, kujifunza na kuazimika kwa kazi au kampeni ya kikundi. Kushiriki kutumia mbinu ni funzo muhimu kwa wafanyikazi wapya na wafanyi kazi wanaojitolea.

**Mfano: Mbinu kwa mafundisho**.
Kituo cha Walioteswa (*Centre for Victims of Torture,CVT*), kilichoanzisha mradi wa mbinu mpya kimeanzisha mkondo wa mazoezi kamambe na usimamizi ya wakimbizi ya kukuza uwezo wa umma na pia kuleta maelewano na ujuzi wa afya ya bongo ili kujenga jamii baada ya ukatili na ukiukaji wa haki za binadamu . CVT imeenzisha mafunzo kwenye kambi za wakimbizi kule Guinea na Sierra Leone. Haya mafunzo inatumia uwezo na usimamizi tawilishi wa hawa wakimbizi. Hawa wakimbizi majuzi wa afya ya akili wameweza kujipatia ujuzi, na pia kusaidia wengine ambao wanastahimili ili kusaidia kujenga jamii yao. Wakati huu, kuna wajuzi wa afya ya akili 122 wanaoshiriki katika huu mradi pamoja na wakimbizi maelfu ambao wanapata huduma tofauti tofauti.

**Uhaji wa kubuni mbinu mpya**
Kubuni mbinu mpya ni muhimu kwa kutekeleza haki za binadamu ulimwenguni. Tukipanua mafikira yetu kimkakati au kimbinu, jamii ya wanaopigania haki za binadamu wapata fursa ya kufanikiwa. Kwa ufupi:

- Mbinu chache yatupa maeneo machache. Mbinu kadha yatupa au yashirikisha maeneo makubwa.

- Kurudia mbinu moja wakati wote yaelekeza utumiaji wakati usiofaa. Mafikira ya mbinu nyumbufu yatupa fursa ya kuathiri shabaha yetu vyema.
- Mbinu iliyotumika mara kwa mara yahimiza wapinzani wetu kujitetea vyema. Unyumbufu wa mbinu unamudu mafunzo na pia miujiza.

Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners,* pages 156-160.

## KUKUZA MBINU AU MIKAKATI MIPYA

*Mpango usiokuwa na kitendo unaambilia patupu,*
*na pia kitendo bila mpango kinaambilia patupu.*

Huu ni msemo wa Sun Tsu aliyetamka haya maneno miaka 2000 iliyopita. Sasa twajua kuwa kuna vitu tatu zilizo tambuliwa na Sun Tzu ambazo zaweza kutupa ushindi katika yale yote twataka kukamilisha.

***Jijue***

Usiamini propaganda yako mwenyewe. Ni lazima ujue nguvu zako na pia malemeo yako, uwezo wako, rasilmali na nguzo zako. Ni muhimu kuelewa uwezo na malemeo ya wenzako ambao mnasaidiana kufanya kazi.

***Mjue mshindani wako***

Usiamini propaganda ya mshindani wako. Pia ni lazima uelewe nguvu, malemeo, na uwezo wa washindani wako. Hii itakuwezesha kuelewa na kuitawanya mbinu au mpango wa washindani wako.

**Yajue mazingira yako**

Mazingira yako ni mahala ambapo utakabiliana na mshindani wako wako. Mfano ni kama wakati, mahala, sheria na mila za mahala ambapo unafanyia kazi.
Ukishamaliza kufahamu na kukusanya maoni haya yote, sasa uko tayari kuunda mpango wako. Mpango wako waweza kuwa kutafuta vitu kama;

- Manuio makuu na shabaha muafaka
- Maeneo na maliasili
- Mbinu utakayo tumia na wakati wake
- Mbinu ni kitendo kimoja kinacho tumiwa kuleta mabadiliko. Ni muhimu kuelewa kuwa mbinu ni moja wapo ya mpango wako.

**KUANZA KAZI**

Ukianza kutumia mbinu za kupigania haki, ni muhimu kuyaweka haya maanani:

**Ungana kufanya kazi na wengine**

Iwezekanavyo, ni muhimu kuleta pamoja watu wa maoni tofauti tofauti ili wajadiliane na wabadilishane maoni na pia wajifunze kutokana na maoni ya wengine.
Ni muhimu kukubaliana na taratibu au sheria ambazo zitaongoza majadiliano. Mfano ni kama:
Kuheshimiana.
Mtu mmoja tuu ndiye ataongea kila wakati.
Maoni yote yakaribishwa.
Matamshi yasiyo ya heshima hayakubaliwi na hata yakinenwa ni lazima yarudiwe kwa njia ya heshima.
Mjadala uendelee kwa heshima

Wanamjadala ni lazima  wakubaliane taratibu za kuingilia kama mmoja wapo wanamjadala anatawala mjadala.

**Jadiliana bila pingamizi au wasiwasi**
Iwezekanapo, kusanya maoni yote. Thibitisha kuwa kila mtu ametoa maoni yake bila kupumbaza au kutupilia mbali maoni mengine kama ngumu kutekeleza au isiyo ya maana. Pia maoni yote yasiwe ya dhalimu, kwani amani ndio nguzo ya uhalali na uaminifu.

Yaandike maoni yote yatakavyotokea ili uchague maoni yale yatakayojadiliwa na yale ambayo hayatajadiliwa. Lakini usiyatupilie mbali maoni yoyote kwa maana utastahili kuyaangaliana na kuyachambua hayo maoni baadaye.

**Andika au nakala hiyo taratibu**
Yaandike maoni yote kwenye waraka au ukuta ili kila mshiriki aifwate taratibu. Maandishi inahakikisha kuwa yale yote yanayojadiliwa yatakumbukwa baadaye na pia kuandika kwapatiana fursa ya kurudia hayo maoni wakati mwingine. Aidha, chambua ponza za kuweka nakala za huu mjadala.

**Hatua ya kwanza:  Tambua shida au tatizo**
- Ni shida gani unayotaka kutatua?
- Ili kuitatua shida hii vyema, andika vidokezo vya hii shida ili uitatue moja kwa moja.
- Shida hiyo yaambatana vipi  na desturi fulani, taasisi, sheria au mtu fulani?
- Iandike shida hiyo kwa sentensi moja fupi.

**Hatua ya pili: Tambua shabaha yako**
- Shabaha yako ni yule mtu, kitu au mahala fulani ambapo unataka kuathiri au kupasa.
- Ni nani au ni nini iliyo na wajibu wa ile shida umetambua?
- Ni nani ambao wanatawilisha hiii shida?
- Kuna taasisi za kutatua hii shida? Kama ziko, ni kwa nini hazichukui hatua ya kutatua hili swala?
- Tambua mojawapo ya shabaha ambazo kikundi chako chataka kuathiri.

**Hatua ya Tatu: Tambua lengo lako**
- Ni athari gani mwataka kutokana na hiyo shida?
- Kwa ufupi, eleza ni tukio gani mnalotaka? Fikiria hivi: kama ungekuwa na nguvu ya kutatua shida zote ulimwenguni, hizo shida zingekuwa zipi? Usijali kuwa umepita kiasi.
- Shabaha zako zakusaidia vipi kutekelza lengo lako?

N.B.  Hili lengo laweza kuwa tofauti na misioni ya shirika au kikundi chako. Ni vyema kuiweka hiyo misioni maanani ili kuhakikisha mkakati au mbinu mlizo chagua zaambatana.

**Hatua ya Nne: Tambua mwandani na mshindani wako**

- Wekelea maanani lengo lako na mbinu zako
- Ni nani mwandani wako?-watu binafsi, vikundi au mashirika- nchini mwako na nchi zingine? Ni kwa sababu gani wangependa kuungana nawe?
- Wapinzani wako ni nani?
- Ni nani waandani na wapinzani wako wasiojulikana? Watu wengi wako kwenye hiki kibengele.
- Kutafuta njia ya kuathiri hivi vikundi itakuwa muhimu mtafutavyo mbinu zenu.

**Hatua Ya Tano: Tambua rasilmali zenu**
Rasilmali ni kitu chochote kinachokusaidia kufikia lengo lako.

- Ni rasilmali gani ulizonazo? Yaweza kuwa vyama vingine viandani, mitandao ya vyama, fedha, na hali ya kisiasa, sheria au maingiano.
- Kikundi chako kina uhusiano gani na shabaha yenu iliyo na uwezo wakutatua shida yenu. Huu uhusiano pia ni rasilmali.
- Wanachama wa kikundi chako pia ni lazima wafikirie vile watakavyojilinda

**Hatua Ya Sita: Tambua mbinu au mkakati wenu**

- Kutambua mkakati wenu unaweza kuwa kufikia uamuzi tofauti tofauti.
- Ukiangalia zile vibengele tulizoongelea, Ni mambo gani ambayo kikundi chako chaweza kuathiri?
- Yaandike mambo hayo ukiweka lengo lako maanani.
- Ni hatua gani ambayo yaweza kufanya mathaara yako kuafikiana na shabaha yako?
- Kuna taratibu ambazo hizi hatua zaweza kutekelezwa moja kwa moja? Au hizi hatua zaweza kutekelezwa mara moja na jitihada zingine? Uko na rasilmali za kutosha?

Ni vyema kujadiliana taratibu za kufikia mbinu na kuweka maanani kuwa mbinu yenu itawaleta karibu na lengo lenu wala sio kutatua shida au tatizo lenu. Hakikisha kuwa taratibu ya matendo yenu ni sawa na lengo la kikundi wala isiwe inawapeleka njia tofauti na lengo.

**Hatua ya Saba: Tambua mkakati au mbinu yenu**
Huu ni wakati wa kuamua ni mbinu gani mtakazo tumia kutekeleza mkakati ambao mumetambua. Mkichagua hizi mbinu, fikiria uwezo wenu na vipaumbele vyenu. Chukua wakati kuwarudia waigishaji wakuu, maeneo, waandani na wapinzani, na pia nguvu zenu, malemeo na rasilmali za kikundi chako na pia washindani wako.

- Andika chini mbinu mnazotambua na mwaweza kufikia
- Ni mbinu gani mwaweza kuhimiza waandani wagumu kuwa waandani wepesi
- Ni mbinu gani zaweza kuhakikisha kuwa wapinzani wagumu wabaki hivyo hivyo au kuwahimiza kuwa waandani?
- Ni mbinu gani zaweza kusimamisha au kulainisha mapingamizi?
- Kikundi chako chaweza kufanya hii kazi kivyake au chahitaji kushirikiana na vikundi vingine?

Chagua mbinu moja inayotoshana na mkakati au lengo lenu ili ijadiliwe.
Mbinu moja itahitaji majadiliano marefu na yaweza kuhitaji kuongezwa mbinu zingine ili itekelezwe kikamilifu.

**Hatua Ya Nane: Kadirisha mbinu moja**

- Jadiliana sababu ya kikundi chako kuchagua hii mbinu.
- Ni sababu gani mbinu hii iko na uwezo wa kusongesha kikundi chako karibu na lengo lenu?
- Mbinu hiii yaweza kukuzwa vipi ili iwe na maathara makuu?
- Mwaweza kuzalisha rasilmali zingine vipi? Ni nani aweza kuungana kufanya kazi na nyinyi? Ni mbinu gani mwahitaji kusadikisha wengine ili waungane kufanya kazi nanyi au wachange rasilmali zao?
- Ni mbinu gani mwaweza kuongezea ili mtekeleze ile mbinu mliochagua? Kuna shabaha ambayo yahitaji kuangaliwa? Ili mfikie shabaha kuu? ( kama kutafuta marafiki kwenye shirika kama mkurugenzi mkuu hajafikiwa kuulizwa kubadilisha sera fulani.
- Mwahitaji usaidizi wa vyama vingine kabla hamjaanza kutekeleza mbinu yenu?

Andika muhtasari wa mbinu zote ziwezekanazo ambazo zaweza kuwasaidia kutekeleza mbinu yenu. Endelea kukadiri rasilmali mlizo nazo.

**Hatua ya Tisa: Kuendekeza mbinu kutoka humu kitabu**

Angalia “Kuendekeza mbinu” (*Adapting Tactics*) kwa maelezo zaidi kuhusu kutumia mbinu

- Chagua mbinu kadhalika mngependa kutumia.
- Mbinu mliochagua yafanana vipi Na hali yenu? Kuna tofauti gani? Ni funzo gani mwaona kutokana na mazoea ya vikundi vingine?
- Kikundi chako kina rasilmali gani zingine ambazo hazijatajwa kwenye hiki kitabu? Hizi rasilmali zaweza kutumika vipi kuhakikisha mbinu yenu inafanya kazi?
- Ni vikwazo gani vingine ambavyo kikundi chako kinatarajia?
- Ni vipi mwaweza kuendekeza hii mbinu kuambatana na hali yenu?
- Mnaitaji maoni gani zaidi na ni nani atayakusanya?

Hii taratibu yaweza kutumiwa kutafuta maoni mapya yatakayo saidia kikundi chako kuafikia lengo lake na pia kuifanya kuwa fundisho la kikundi chako. Pia itakuwezesha kukuza ujuzi wa uchambuzi utakao kusaidia kukadiri mbinu au mkakati wenu.

Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners*, pages 162-163.

**KUSAMBAZA MBINU YAKO: A SAMPULI YA KIPAJI CHA MBINU**

Mradi wa mbinu mpya (*New Tactics Project*) unashugulikia kusoma na kufundisha mbinu mpya. Hatutaki ufikirie juu ya kazi yako kwa upande wa mbinu na pia ujifunze mbinu mpya kutoka humu kitabuni, bali pia usambaze mbinu zako kwa wengine. Kusambaza mbinu yafaidisha wale walioanzisha mbinu ( kwa kujenga ujuzi wao wa uongozi na kipaji ) na pia wale ambao wanafundisha.

Mwongozo mfupi wa dakika 40 za kipaji ya mbinu zako unafwata. Tumia huu mwongozo kukusaidia kuchagua yale mambo yatakayo saidia kikundi chako kuelewa na kutekeleza mbinu yako.

**Kwa Dakika moja**
***Tamka mbinu Yako.***
Anza mafundisho yako kwa kueleza kwa ufupi mbinu yako. Kumbuka kulenga shabaha yako kwa mbinu yako wala sio kwa shida au tatizo au muktadha. Rudia maana ya mbinu kwa p.21 na usome "*The Need for New Tactics*" p.12 ili usiwe na wasi wasi wowote juu ya hili jambo -maana ya mbinu.

Pia fikiria njia sisitizi ya kueleza kikundi chako ni kwa nini hii mbinu ni ya kipekee, muhimu au ya kufana. Waweza kusema hadithi ama uulize swali litakalo chemsha bongo za wasikilizaji wako.

**Dakika 5**
***Eleza Muktadha***
Wataka wasikilizaji wako waelewe ni kwa nini hii mbinu ilitumika kwa hii hali yako. Wasaidie kuelewa kwa njia ifuatayo:

- Eleza mambo ya maingiano ya wakati huu au ya kale yaliyohitaji mwitikio, sana sana yale yatakayosaidia wengine kuelewa mbinu yako.
- Eleza utaratibu ambao huu mwitikio ulipangiliwa
- Eleza matokeo unayonuia kwa kutumia hii mbinu i.e. shabaha na malengo
- Kwa ufupi, eleza mkakati uliotumiwa na vile mbinu hiii yaambatana na huo mkakati
- Sio lazima uchukue mda mrefu kueleza haya maswala lakini kumbuka kuyaguzia.

**Dakika 20**
***Eleza vile Mbinu Yatumika***
Hii ndio kiini ya kipaji. Kumbuka unapatia wasikilizaji wako maarifa muhimu watakayohitaji kutekeleza mbinu yako katika hali zao.
Eleza moja kwa moja vile ulitekeleza hii mbinu.Tungependelea utumie kesi moja maalum kama mfano. Fikiria mwenzako anayetoka nchi nyingine atastahili kujua nini? Ataanza vipi? Ni watu ngapi watajihusisha? Wanahitaji usaidizi gani? Wanahitaji rasilmali gani?

Kumbuka kueleza moja kwa moja!

**Dakika 7**
***Rudia maendeleo ya hiyo mbinu***
Ongea juu ya shabaha: Mbinu hii yatarajiwa kuathiri tabia, taasisi, sera au mtu gani? Kumbuka kuwa kwaweza kuwa na shabaha ya kwanza na pia shabaha ya mwisho.

Eleza matokeo yakini. Walioshughulikia hili swala wanaeleza vipi matokeo wanayotarajia na pia maathara? Tumia misemo au maneno ya wale walioshughulikia hili swala.

**Dakika 7**
***Eleza mafunzo uliyopata na vile mbinu hii yaweza kutumika kwingine***
Eleza mafunzo uliyopata ukitekeleza hii mbinu. Nini ilifanya kazi? Ni nini ungefanya tofauti? Ni mawaidha au mapendekezo gani ungepeana kwa wengine?
Kwa mazoea yako, ni mambo gani ungependa yawekwe maanani kabla ya kutekeleza hii mbinu? Kuna malemeo gani?

Kama unajua matumizi mengine ya mbinu hii, Kwa ufupi, eleza vile ilitekelezwa kitofauti na ni kwa nini.

Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners*, page 161.

**Kuendekeza Mbinu Mpya**

Mbinu ambazo hiki kitabu chazungumzia kilinuia kukupa matumaini ndivyo ufikirie njia mpya ya kusaidia kikundi chako kufanya kazi yake. Twatumaini kuwa utapata mbinu zingine za kutumia zinazoambatana na mazingira au hali yako.

Tukisema kuwa mbinu zaweza kuhamishwa, twamaanisha kuwa hizo mbinu zaweza kutumika kwa nchi zingine au mazingira mengine licha ya hayo ambapo mbinu hiyo ilitumika.

Ni lazima ukadiri mazingira yako wewe mwenyewe na pia rasilmali zako. Pengine ungependa kuchanganya mbinu mbili au waweza kupata kuwa vibengele vya hiyo mbinu vyatumika wala sio mbinu yote.

Haya maswala yaweza kukusaidia kukadiri na kuendekeza mbinu mpya kwa hali yako.

- Mbinu hii ni sawa kwa jambo langu na hali yangu?
- Naweza kujadiliana hili swala na nani mwingine?
- Naweza kuongea na vikundi vingine vipi?
- Nimeshaona au kutumia mbinu ingine kama hii?
- Hiii mbinu ilifaulu?
- Kwa nini ilifaulu au kufeli?
- Mbinu hii itanisaidia vipi kuafikia lengo langu?
- Naweza kupata maadhara ninayonuia kwa shabaha?
- Hii mbinu ishatumiwa mara nyingine kwa shabaha kama yangu?
- Nahitaji rasilmali gani?
- Niko na rasilmali gani?
- Nitapata vipi zile rasilmali sina?
- Nitaongea na nani kuhusu hii mbinu?
- Nitaunda mitandao gani ili niweze kutumia mbinu hii?
- Nitaunda hizo mitandao vipi?
- Wapinzani wangu watachukua hii mbinu yangu vipi?
- Mbinu hii ina ponzi gani kwangu na kwa kikundi changu?
- Niko tayari kukutana na hii ponza?
- Naweza kupunguza vipi ponza za kutumia mbinu hii?
- Naweza kutumia vibengele fulani vya hii mbinu?
- Naweza kutumia hii mbinu pamoja na mbinu zingine?
- Niko na mpango gani mwingine?
- Niko na mpango gani ikiwa hii mbinu haiendelei vile ninavyo tarajia?

Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners*, pages 8-9.

## UTANGULIZI

Katika miongo mbili zilizopita ulimwengu umeona mwanzo mpya katika eneo la haki za kibinadamu ambapo umuhimu wa sheria za kimataifa na pia mafikira ya wananchi imetambulika. Kwa upande wa sheria za kimataifa, mbinu mpya zimegeuza mafikira yetu na vile ambavyo kutekeleza haki .Vile vile, mafikira mapya na ule moyo wa watu binafsi na vikundi kuleta mageuzi umegeuza mafikira yetu kuhusu yale ambayo twaweza kufanya kwa uwanja wa haki za kibinadamu- na kwa hivyo yale ambayo twaweza kutimiza.

Kote duniani, mashambani na serikalini na pia kwenye maeneo makuu ya sheria za kimataifa, watu wanaunda na kutumia, mbinu na njia mbali mbali za kuhakikisha kwamba kazi yao yatekelezwa vyema. Mradi wa Mbinu Mpya Kwa Haki Za Kibinadamu (*New Tactics in Human Rights Project*) umezichukua hizi mbinu mpya na kuzisambaza kwa wengine ambao wanafanya kazi kwa uwanja wa haki za kibinadamu. Mwakaribishwa nyote kushangilia hii kazi na kutumia hiki kitabu kilicho mikononi mwenyu kama chombo maalum.

Nikifikiria kazi yangu ambayo nafanya, naona fursa mpya ya kuwapa haki wale ambao haki zao zimekiuka. Kuanzishwa kwa koti ya jinai ya iliyokuwa Yugoslavia na Rwanda, ambayo iliyokuwa koti ya kwanza ya jinai za vita imeleta mafikira mapya kwenye mataifa na pia zilifungua milango mipya za haki. Wajuzi waliuotumika kwenye hizo koti kutoka nchi mbali mbali walitenda kile ambacho hakijatendwa awali- kuunda sheria mpya na kuanzisha desturi mpya kwa kushtaki washtakiwa na mashtaka ambayo yalikuwa hayajatumika na nchi yeyote ulimwenguni. Hayo yote yalizaa mbinu mpya ambazo zilifungua njia ya mbinu kuu- Koti ya Jinai ya Kimataifa ( *International Criminal Court).* Koti hii sasa yatupatia chombo cha kulinda na kutekeleza haki bila kujali ni wapi ama ni nani aliye kiuka hizo haki za kibinadamu.

Mbinu mpya pia ilitumika zile nyakati za koti ya jinai ya iliyokua Yugoslavia kwa kushtaki waliokuwa polisi wa Bosnia na mashtaka ya Kunajisi wanawake waislamu wa Bosnia. Hii mbinu imewezesha sheria na haki kutekelezwa mara mingi.

Miaka kumi iliyopita, wanasheria wangepumbaza swala la kumushtaki aliyekuwa Rais Agusto Pinochet. Wakati huo, wahalifu _walikuwa wanajidai wakizurura kote ulimwenguni bila pingamizi. Kushikwa na kushtakiwa kwa Pinochet kulibadilisha mafikira ya wanaopigania haki za kibinadamu.

Nashangilia harakati za wanaopigania haki za kibinadamu kutumia koti za kitaifa na za kimataifa kujulisha ulimwengu kesi za jinai popote ambazo zinatokea. Lakini haya ni chache tu kwa zile mbinu mpya zinazo tumika kupigania haki za kibinadamu popote ulimwenguni.

Najivunia kuungana na mradi wa mbinu mpya kwa haki za kibinadamu ( *New Tactics in Human Rights Project*) kwa kutoa hii maktaba. Na ingawa haiwezi kusemekana kuwa kamilifu, hii ni maktaba iliyojaa mawazo mapya na mbinu mpya ambazo zaweza kusaidia yeyote kutekeleza kazi yake.

-Jaji Richard J. Goldstone
Jaji mstaaafu wa Koti ya Katiba ya Afrika Kusini
Mshtaki mkuu wa Koti ya Jinai ya iliyokuwa Yugoslavia na Rwanda
Mwenye kiti wa Koti ya Kimataifa ya Kosovo
Mwenyekiti wa Tume ya Kimataifa ya Kuchunguza Ujangili iliyoanzishwa na International Bar Association.

--------------------------------------------------

Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners*, pages 156-160.

# KUKUZA MBINU AU MIKAKATI MIPYA

*Mpango usiokuwa na kitendo unaambilia patupu,*
*na pia kitendo bila mpango kinaambilia patupu.*

Huu ni msemo wa Sun Tsu aliyetamka haya maneno miaka 2000 iliyopita. Sasa twajua kuwa kuna vitu tatu zilizo tambuliwa na Sun Tzu ambazo zaweza kutupa ushindi katika yale yote twataka kukamilisha.

***Jijue***

Usiamini propaganda yako mwenyewe. Ni lazima ujue nguvu zako na pia malemeo yako, uwezo wako, rasilmali na nguzo zako. Ni muhimu kuelewa uwezo na malemeo ya wenzako ambao mnasaidiana kufanya kazi.

***Mjue mshindani wako***

Usiamini propaganda ya mshindani wako. Pia ni lazima uelewe nguvu, malemeo, na uwezo wa washindani wako. Hii itakuwezesha kuelewa na kuitawanya mbinu au mpango wa washindani wako.

**Yajue mazingira yako**

Mazingira yako ni mahala ambapo utakabiliana na mshindani wako wako. Mfano ni kama wakati, mahala, sheria na mila za mahala ambapo unafanyia kazi.
Ukishamaliza kufahamu na kukusanya maoni haya yote, sasa uko tayari kuunda mpango wako. Mpango wako waweza kuwa kutafuta vitu kama;

- Manuio makuu na shabaha muafaka
- Maeneo na maliasili
- Mbinu utakayo tumia na wakati wake
- Mbinu ni kitendo kimoja kinacho tumiwa kuleta mabadiliko. Ni muhimu kuelewa kuwa mbinu ni moja wapo ya mpango wako.

## KUANZA KAZI

Ukianza kutumia mbinu za kupigania haki, ni muhimu kuyaweka haya maanani:

**Ungana kufanya kazi na wengine**

Iwezekanavyo, ni muhimu kuleta pamoja watu wa maoni tofauti tofauti ili wajadiliane na wabadilishane maoni na pia wajifunze kutokana na maoni ya wengine.
Ni muhimu kukubaliana na taratibu au sheria ambazo zitaongoza majadiliano. Mfano ni kama:
Kuheshimiana.
Mtu mmoja tuu ndiye ataongea kila wakati.
Maoni yote yakaribishwa.
Matamshi yasiyo ya heshima hayakubaliwi na hata yakinenwa ni lazima yarudiwe kwa njia ya heshima.
Mjadala uendelee kwa heshima
Wanamjadala ni lazima wakubaliane taratibu za kuingilia kama mmoja wapo wanamjadala anatawala mjadala.

**Jadiliana bila pingamizi au wasiwasi**

Iwezekanapo, kusanya maoni yote. Thibitisha kuwa kila mtu ametoa maoni yake bila kupumbaza au kutupilia mbali maoni mengine kama ngumu kutekeleza au isiyo ya maana. Pia maoni yote yasiwe ya dhalimu, kwani amani ndio nguzo ya uhalali na uaminifu.

Yaandike maoni yote yatakavyotokea ili uchague maoni yale yatakayojadiliwa na yale ambayo hayatajadiliwa. Lakini usiyatupilie mbali maoni yoyote kwa maana utastahili kuyaangaliana na kuyachambua hayo maoni baadaye.

**Andika au nakala hiyo taratibu**
Yaandike maoni yote kwenye waraka au ukuta ili kila mshiriki aifwate taratibu. Maandishi inahakikisha kuwa yale yote yanayojadiliwa yatakumbukwa baadaye na pia kuandika kwapatiana fursa ya kurudia hayo maoni wakati mwingine. Aidha, chambua ponza za kuweka nakala za huu mjadala.

**Hatua ya kwanza:  Tambua shida au tatizo**

- Ni shida gani unayotaka kutatua?
- Ili kuitatua shida hii vyema, andika vidokezo vya hii shida ili uitatue moja kwa moja.
- Shida hiyo yaambatana vipi  na desturi fulani, taasisi, sheria au mtu fulani?
- Iandike shida hiyo kwa sentensi moja fupi.

**Hatua ya pili: Tambua shabaha yako**

- Shabaha yako ni yule mtu, kitu au mahala fulani ambapo unataka kuathiri au  kupasa.
- Ni nani au ni nini iliyo na wajibu wa ile shida umetambua?
- Ni nani ambao wanatawilisha hiii shida?
- Kuna taasisi za kutatua hii shida? Kama ziko, ni kwa nini hazichukui hatua ya kutatua hili swala?
- Tambua mojawapo ya shabaha ambazo kikundi chako chataka kuathiri.

**Hatua ya Tatu: Tambua lengo lako**

- Ni athari gani mwataka kutokana na hiyo shida?
- Kwa ufupi, eleza ni tukio gani mnalotaka? Fikiria hivi: kama ungekuwa na nguvu ya kutatua shida zote ulimwenguni, hizo shida zingekuwa zipi? Usijali kuwa umepita kiasi.
- Shabaha zako zakusaidia vipi kutekelza lengo lako?

N.B.  Hili lengo laweza kuwa tofauti na misioni ya shirika au kikundi chako. Ni vyema kuiweka hiyo misioni maanani ili kuhakikisha mkakati au mbinu mlizo chagua zaambatana.

**Hatua ya Nne: Tambua mwandani na mshindani wako**

- Wekelea maanani lengo lako na mbinu zako
- Ni nani mwandani wako?-watu binafsi, vikundi au mashirika- nchini mwako na nchi zingine? Ni kwa sababu gani wangependa kuungana nawe?
- Wapinzani wako ni nani?
- Ni nani waandani na wapinzani wako wasiojulikana? Watu wengi wako kwenye hiki kibengele.
- Kutafuta njia ya kuathiri  hivi vikundi itakuwa muhimu mtafutavyo mbinu zenu.

**Hatua Ya Tano: Tambua rasilmali zenu**
Rasilmali ni kitu chochote kinachokusaidia kufikia lengo lako.

- Ni rasilmali gani ulizonazo? Yaweza kuwa vyama vingine viandani, mitandao ya vyama, fedha, na hali ya kisiasa, sheria au maingiano.
- Kikundi chako kina uhusiano gani na shabaha yenu iliyo na uwezo wakutatua shida yenu. Huu uhusiano pia ni rasilmali.
- Wanachama wa kikundi chako pia ni lazima wafikirie vile watakavyojilinda

**Hatua Ya Sita: Tambua mbinu au mkakati wenu**

- Kutambua mkakati wenu unaweza kuwa kufikia uamuzi tofauti tofauti.
- Ukiangalia zile vibengele tulizoongelea, Ni mambo gani ambayo kikundi chako chaweza kuathiri?
- Yaandike mambo hayo ukiweka lengo lako maanani.
- Ni hatua gani ambayo yaweza kufanya mathaara yako kuafikiana na shabaha yako?
- Kuna taratibu ambazo hizi hatua zaweza kutekelezwa moja kwa moja? Au hizi hatua zaweza kutekelezwa mara moja na jitihada zingine? Uko na rasilmali za kutosha?

Ni vyema kujadiliana taratibu za kufikia mbinu na kuweka maanani kuwa mbinu yenu itawaleta karibu na lengo lenu wala sio kutatua shida au tatizo lenu. Hakikisha kuwa taratibu ya matendo yenu ni sawa na lengo la kikundi wala isiwe inawapeleka njia tofauti na lengo.

**Hatua ya Saba: Tambua mkakati au mbinu yenu**

Huu ni wakati wa kuamua ni mbinu gani mtakazo tumia kutekeleza mkakati ambao mumetambua. Mkichagua hizi mbinu, fikiria uwezo wenu na vipaumbele vyenu. Chukua wakati kuwarudia waigishaji wakuu, maeneo, waandani na wapinzani, na pia nguvu zenu, malemeo na rasilmali za kikundi chako na pia washindani wako.

- Andika chini mbinu mnazotambua na mwaweza kufikia
- Ni mbinu gani mwaweza kuhimiza waandani wagumu kuwa waandani wepesi
- Ni mbinu gani zaweza kuhakikisha kuwa wapinzani wagumu wabaki hivyo hivyo au kuwahimiza kuwa waandani?
- Ni mbinu gani zaweza kusimamisha au kulainisha mapingamizi?
- Kikundi chako chaweza kufanya hii kazi kivyake au chahitaji kushirikiana na vikundi vingine?

Chagua mbinu moja inayotoshana na mkakati au lengo lenu ili ijadiliwe.
Mbinu moja itahitaji majadiliano marefu na yaweza kuhitaji kuongezwa mbinu zingine ili itekelezwe kikamilifu.

**Hatua Ya Nane: Kadirisha mbinu moja**

- Jadiliana sababu ya kikundi chako kuchagua hii mbinu.
- Ni sababu gani mbinu hii iko na uwezo wa kusongesha kikundi chako karibu na lengo lenu?
- Mbinu hiii yaweza kukuzwa vipi ili iwe na maathara makuu?
- Mwaweza kuzalisha rasilmali zingine vipi? Ni nani aweza kuungana kufanya kazi na nyinyi? Ni mbinu gani mwahitaji kusadikisha wengine ili waungane kufanya kazi nanyi au wachange rasilmali zao?
- Ni mbinu gani mwaweza kuongezea ili mtekeleze ile mbinu mliochagua? Kuna shabaha ambayo yahitaji kuangaliwa? Ili mfikie shabaha kuu? ( kama kutafuta marafiki kwenye shirika kama mkurugenzi mkuu hajafikiwa kuulizwa kubadilisha sera fulani.
- Mwahitaji usaidizi wa vyama vingine kabla hamjaanza kutekeleza mbinu yenu?

Andika muhtasari wa mbinu zote ziwezekanazo ambazo zaweza kuwasaidia kutekeleza mbinu yenu. Endelea kukadiri rasilmali mlizo nazo.

**Hatua ya Tisa: Kuendekeza mbinu kutoka humu kitabu**

Angalia "Kuendekeza mbinu" (*Adapting Tactics*) kwa maelezo zaidi kuhusu kutumia mbinu

- Chagua mbinu kadhalika mngependa kutumia.

- Mbinu mliochagua yafanana vipi Na hali yenu? Kuna tofauti gani? Ni funzo gani mwaona kutokana na mazoea ya vikundi vingine?
- Kikundi chako kina rasilmali gani zingine ambazo hazijatajwa kwenye hiki kitabu? Hizi rasilmali zaweza kutumika vipi kuhakikisha mbinu yenu inafanya kazi?
- Ni vikwazo gani vingine ambavyo kikundi chako kinatarajia?
- Ni vipi mwaweza kuendekeza hii mbinu kuambatana na hali yenu?
- Mnaitaji maoni gani zaidi na ni nani atayakusanya?

Hii taratibu yaweza kutumiwa kutafuta maoni mapya yatakayo saidia kikundi chako kuafikia lengo lake na pia kuifanya kuwa fundisho la kikundi chako. Pia itakuwezesha kukuza ujuzi wa uchambuzi utakao kusaidia kukadiri mbinu au mkakati wenu.

---------------------------------------------------

Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners*, page 161.

**Kuendekeza Mbinu Mpya**

Mbinu ambazo hiki kitabu chazungumzia kilinuia kukupa matumaini ndivyo ufikirie njia mpya ya kusaidia kikundi chako kufanya kazi yake. Twatumaini kuwa utapata mbinu zingine za kutumia zinazoambatana na mazingira au hali yako.

Tukisema kuwa mbinu zaweza kuhamishwa, twamaanisha kuwa hizo mbinu zaweza kutumika kwa nchi zingine au mazingira mengine licha ya hayo ambapo mbinu hiyo ilitumika.

Ni lazima ukadiri mazingira yako wewe mwenyewe na pia rasilmali zako. Pengine ungependa kuchanganya mbinu mbili au waweza kupata kuwa vibengele vya hiyo mbinu vyatumika wala sio mbinu yote.

Haya maswala yaweza kukusaidia kukadiri na kuendekeza mbinu mpya kwa hali yako.

- Mbinu hii ni sawa kwa jambo langu na hali yangu?
- Naweza kujadiliana hili swala na nani mwingine?
- Naweza kuongea na vikundi vingine vipi?
- Nimeshaona au kutumia mbinu ingine kama hii?
- Hiii mbinu ilifaulu?
- Kwa nini ilifaulu au kufeli?
- Mbinu hii itanisaidia vipi kuafikia lengo langu?
- Naweza kupata maadhara ninayonuia kwa shabaha?
- Hii mbinu ishatumiwa mara nyingine kwa shabaha kama yangu?
- Nahitaji rasilmali gani?
- Niko na rasilmali gani?
- Nitapata vipi zile rasilmali sina?
- Nitaongea na nani kuhusu hii mbinu?
- Nitaunda mitandao gani ili niweze kutumia mbinu hii?
- Nitaunda hizo mitandao vipi?
- Wapinzani wangu watachukua hii mbinu yangu vipi?
- Mbinu hii ina ponzi gani kwangu na kwa kikundi changu?
- Niko tayari kukutana na hii ponza?
- Naweza kupunguza vipi ponza za kutumia mbinu hii?

- Naweza kutumia vibengele fulani vya hii mbinu?
- Naweza kutumia hii mbinu pamoja na mbinu zingine?
- Niko na mpango gani mwingine?
- Niko na mpango gani ikiwa hii mbinu haiendelei vile ninavyo tarajia?

------------------------------------------------------

Source: *New Tactics in Human Rights: A Resource for Practitioners*, pages 162-163.

**KUSAMBAZA MBINU YAKO: A SAMPULI YA KIPAJI CHA MBINU**

Mradi wa mbinu mpya (*New Tactics Project*) unashugulikia kusoma na kufundisha mbinu mpya. Hatutaki ufikirie juu ya kazi yako kwa upande wa mbinu na pia ujifunze mbinu mpya kutoka humu kitabuni, bali pia usambaze mbinu zako kwa wengine. Kusambaza mbinu yafaidisha wale walioanzisha mbinu ( kwa kujenga ujuzi wao wa uongozi na kipaji ) na pia wale ambao wanafundisha.

Mwongozo mfupi wa dakika 40 za kipaji ya mbinu zako unafwata. Tumia huu mwongozo kukusaidia kuchagua yale mambo yatakayo saidia kikundi chako kuelewa na kutekeleza mbinu yako.

**Kwa Dakika moja**
***Tamka mbinu Yako.***
Anza mafundisho yako kwa kueleza kwa ufupi mbinu yako. Kumbuka kulenga shabaha yako kwa mbinu yako wala sio kwa shida au tatizo au muktadha. Rudia maana ya mbinu kwa p.21 na usome "*The Need for New Tactics*" p.12 ili usiwe na wasi wasi wowote juu ya hili jambo -maana ya mbinu.

Pia fikiria njia sisitizi ya kueleza kikundi chako ni kwa nini hii mbinu ni ya kipekee, muhimu au ya kufana. Waweza kusema hadithi ama uulize swali litakalo chemsha bongo za wasikilizaji wako.

**Dakika 5**
***Eleza Muktadha***
Wataka wasikilizaji wako waelewe ni kwa nini hii mbinu ilitumika kwa hii hali yako. Wasaidie kuelewa kwa njia ifuatayo:

- Eleza mambo ya maingiano ya wakati huu au ya kale yaliyohitaji mwitikio, sana sana yale yatakayosaidia wengine kuelewa mbinu yako.
- Eleza utaratibu ambao huu mwitikio ulipangiliwa
- Eleza matokeo unayonuia kwa kutumia hii mbinu i.e. shabaha na malengo
- Kwa ufupi, eleza mkakati uliotumiwa na vile mbinu hiii yaambatana na huo mkakati
- Sio lazima uchukue mda mrefu kueleza haya maswala lakini kumbuka kuyaguzia.

**Dakika 20**
***Eleza vile Mbinu Yatumika***
Hii ndio kiini ya kipaji. Kumbuka unapatia wasikilizaji wako maarifa muhimu watakayohitaji kutekeleza mbinu yako katika hali zao.
Eleza moja kwa moja vile ulitekeleza hii mbinu.Tungependelea utumie kesi moja maalum kama mfano. Fikiria mwenzako anayetoka nchi nyingine atastahili kujua nini? Ataanza vipi? Ni watu ngapi watajihusisha? Wanahitaji usaidizi gani? Wanahitaji rasilmali gani?

Kumbuka kueleza moja kwa moja!

**Dakika 7**
***Rudia maendeleo ya hiyo mbinu***
Ongea juu ya shabaha: Mbinu hii yatarajiwa kuathiri tabia, taasisi, sera au mtu gani? Kumbuka kuwa kwaweza kuwa na shabaha ya kwanza na pia shabaha ya mwisho.

Eleza matokeo yakini. Walioshughulikia hili swala wanaeleza vipi matokeo wanayotarajia na pia maathara? Tumia misemo au maneno ya wale walioshughulikia hili swala.

**Dakika 7**
***Eleza mafunzo uliyopata na vile mbinu hii yaweza kutumika kwingine***
Eleza mafunzo uliyopata ukitekeleza hii mbinu. Nini ilifanya kazi? Ni nini ungefanya tofauti? Ni mawaidha au mapendekezo gani ungepeana kwa wengine?
Kwa mazoea yako, ni mambo gani ungependa yawekwe maanani kabla ya kutekeleza hii mbinu? Kuna malemeo gani?

Kama unajua matumizi mengine ya mbinu hii, Kwa ufupi, eleza vile ilitekelezwa kitofauti na ni kwa nini.
----------------------------------------------------

Source: The Need for New Tactics (Guide)
An online resource from the New Tactics website: http://www.newtactics.org/file.php?ID=948

**UHAJI WA MBINU MPYA**
**NYENDO MPYA ZA HAKI ZA BINADAMU**

Miongo iliyopita imeiona mienendo mipya ya haki za binadamu ikifanikiwa kustawisha haki za binadamu na pia kutafuta njia ya kuzilinda. Mfano ni:

- Kulaani kuteswa
- Kulinda haki za wanawake na watoto
- Harakati halali za kisiasa
- Wafungwa wa kisiasa wamelindwa na kuachiliwa huru
- Kufuatilia kiada za haki za binadamu

Hatuwezi kuzidi kuhimiza umuhimu wa haya majilio au mapato na vile ilikuwa vigumu kuyatekeleza.

**Mbinu kwa nyendo za haki za binadamu**
Mbinu tatu zilichangia kwa haya maendeleo:

1. Kustawisha desturi za kimataifa ambazo ziliunda jamii ya kanuni, mapatano na kiada
2. Kuchunguza kutimizwa kwa kiada
3. Kulaani au kuaibisha vitendo vya serikali au kutotenda ikiwa kiada zakiukwa

**Upungufu**
Ni wazi kuwa hizi mbinuzimeleta maendeleo makuu na inapasa ziendelee kunusuriwa na kufwatiliwa. Ni wazi pia kuna malemeo makuu kwa yale twaweza kufanya kutumia hii njia na sio maridhawa kuchambua maswala makuu kutumia njia hii.

**Kueneza hii nyendo**
Inasemekana kuwa huu mradi wa kuendeleza haki za binadamu wahitaji kuunda uwanja pana ambao utachukua watu wengi kutoka sekta zote za umma.

Pia yahitaji kuendeleza mikakati kamilifu ambazo zaweza kutekelezwa kutumia mbinu tofauti tofauti ambazo zinatumuka.

**Mizuka ya mbinu mpya**
Kote ulimwenguni, wanaharakati wa haki za binadamu waliojitolea wameanzisha kazi hii:

- Kukuza mbinu mpya
- Kujenga mitandao isiyo tarajiwa
- Kujifunza kutoka kwa sekta zisizo tarajiwa

Mradi wa mbinu mpya wa haki za binadamu (*New Tactics for Human Rights Project*) una nia ya kuwaleta pamoja hawa wazushi na kutumainisha wengine na kazi yao. Zikiwekwa pamoja, hizi visa zawakilisha mizuka ya yale tunayoweza kutekeleza kwa upande wa haki za binadamu.

**Faida Ya Kufikiria Kimbinu**
Katika msomo huu, tuna tahsarisha sababu sita ambazo tunaamini zitasaidia kujenga nyendo sawa ya haki za binadamu:

1. Yale ambayo tunajua inaathiri yale tunaamini twaweza kufanya; mbinu zinasaidia kuamua mkakati
2. Mbinu tofauti yaambatana na shabaha tofauti
3. Mbinu tofauti zinavutia maeneo tofauti
4. Unyumbufu wa mbinu ni chanzo cha miujiza
5. Mbinu zafunza washiriki na wazhunguzi njinsi ya kujishughulisha ulimwenguni
6. Mbinu ni njia ya kufunza na kushughulisha washiriki na waandani kwenye kazi ya kikundi

**1. Mbinu zapenya njia mpya**

Yale ambayo twajua kufanya yathiri yale tunaamini twaweza kufanya; mbinu zasaidia kuchagua mkakati. Tukifikiria vile tutakavyofanya, twaweza kuzuia maoni yetu kwa yale ambayo twaweza kutekeleza. Historia imejaa na mifano ambayo jawabu moja inatumika mara kwa mara bila ushindi, au ambapo mbinu mpya inachukuwa mahala pa mbinu mzee.

**Mfano: Mbinu yaamua mkakati**

BAOBAB ya Haki za Akina Mama (BAOBAB) na (*Civil Resource and Documentation Centre-CIRDDOC)* kule Nigeria ilikuwa inapigania kujulisha umma juu ya uhasama dhidi ya wanawake. Watu wachache huko Nigeria waliamini kuwa wanawake wanastahimili uhasama. Serikali, polisi na hata vyombo vya habari havikutilia maanai swala hili.

Vyama visivyo vya serikali ( NGO) vilihabarishwa maathara ya tume ya Vienna na Tokyo na takabadhi ambazo zilivutia. Waliamua kujaribu mbinu mpya na walipanga tume duni ya uhasama dhidi ya wanawake. CIRDDOC ilitengeneza majaribio na tume duni kwenye jimbo la Amambra huko Nigeria ambayo ilikuwa inashughulikia swala la ukiukaji wa haki za binadamu. Tukio hili lilichukuliwa kama ushindi, kwa sababu watu wengi walihudhuria na ikasaidia kuleta majadiliano kwenye swala la kukiuka haki za binadamu kwa jumla na haki za akina mama. Mbinu ya kuunda tume duni ilileta matumaini.

Baadaye, Tume ya Taifa ya Nigeria Inayoshughulikia Uhasama Dhidi ya Wanawake (*Nigeria National Tribunal on Violence Against Women*) iliyoundwa ilivutia takabadhi ya wapasha habari na umma. Baada ya tume, hili swala lilisongelea kwenye ajenda ya umma na ikafungua njia timamu za kutumia mbinu tofauti kama kufundisha umma na mkandamizo. Tukio hili ni muhimu kwa pigano hili refu la kustawisha na kuhifadhi haki za akina mama kama haki za binadamu huko Nigeria.

**2. Mbinu Zaathiri Shabaha Vingine**
Mbinu tofauti zatumika vyeme kwa shabaha tofauti. Ni lazima tujifunze kuzimudu mbinu zetu kuambatana na shabaha zetu tukitafuta zile ambazo zitatupa matokeo kamili. Mbinu zikifeli kuathiri shabaha zetu, ni lazima tuunde mbinu mpya zitakazo tusaidia kufanya kazi.

**Mfano: Mbinu Zaathiri Shabaha Vingine**
Tume ya Haki za Kibinadamu na Uongofu Tekelezi (The Commission on Human Rights and Adminstrative Justice- CHRAJ) kule Ghana iliamua kushughulikia swala la Trokosi, mila inayotumika kwenye pande Fulani za nchi ambapo waganga wanaweka akina mama au wasichana kama watumwa ili kuomba msamaha kwa yale makosa au dhambi za jamaa zao.Hii tume ilitambua kuwa kutumia sheria kukomesha haya makosa haingefanikiwa na hata ingelazimisha hawa waganga kuendelea nah ii mila kisirisiri. Tume ilichagua kuzungumza na hawa waganga ikitumia njia tofauti. Ilitumia wazee wa kijiji na wataifa kwa majadiliano na wahalifu, wahanga, viongozi wengine wa umma na umma kwa jumla kuleta maelewano juu ya hiyo mila na pia ikipatiana abudi na njia za kuitupilia mbali hiyo mila bila kupoteza cheo. Kwa sababu walielewa shabaha yao, waliweza kuchagua mbinu zinazofaa. Wakati huu, zaidi ya wanawake na watoto 3,000 wameweza kuokolewa kutokana na mila ya Trokosi.

**3. Mbinu zajenga Maeneo**
Ikiwa jamii ya wanaopigania haki za kibinadamu yatumia mbinu moja au mbili tuu kushughulisha umaa itajikuta inavutia watu wachache tu ambao wanaelewa hiyo mbinu.Watu ambao wamezoea ubeberu wamejitenga na umma.Kuwashirikisha watu kama hawa, ni lazima tutumie mbinu zinazoambatana na mazoea au desturi zao.

**Mfano: Kujenga Maeneo**
*A mnesty Internationa (AI)* huko Netherlands ilionelea kuwa wale ambao walishiriki kwa mikakati yao ya Vitendo vya Dharura (Urgent Action) walikuwa wametimia miaka 30 na juu, lakini walitaka kuwasirikisha vijana pia. AI-Netherlands ilitumia maandishi kutumia teknologia ya simu ya mkono (Text Messaging Technology) kuwavutia na kushughulisha hawa vijana kwenye kampeni dhidhi ya kuteswa. Katika harakati za kuwafikia hili eneo, walisambaza kampeni zao kwenye tafrija za muziki na pia mahala pengine ambapo vijana hukusanyika.

**4. Unyumbufu wa Mbinu au Mikakati**
Unyumbufu wa mbinu ni chanzo cha miujiza.
Tukizidi kurudia zile mbinu ambazo tumetumia hapo awali, wapinzani wetu wanazoea hizo mbinu. Kumudu mbinu mpya zinasaidia kuweka wapinzani wetu macho. Unyumbufu unakuza mafunzo kwenye pande zote.

**Mfano:  Unyumbufu wa Mbinu**
Otpor! Chama cha wanafundi huko Serbia kilitumia mbinu flexibility kwenye harakati za kupigana dhidi ya utumwa kwenye milki ya Milosevic. Waliuita huu msogeo “Plan B.” Serikali ya Serbia ilipoanza kuwashika waandamizi,Otpor! Ilipanga maandamano mengine kwenye stesheni za polisi ambapo waandamizi walioshikwa walikuwa wamewekwa. Hii ilipatia watu fursa ya kutupilia mbali uwoga wa kushiki kwenye maandamano. Pia ilisaidia kuvunja nguvu za milki ya Milosevic.

**5. Mbinu Zafunza Mashughuliko**
Mbinu zafunza washiriki jinsi ya kujishughulisha ulimwenguni. Tukiendelea kufanya mazoezi, mishipa yajifunza kusonga ikiupatia bongo fursa ya kupanga na kumudu njia mpya.Tukiendelea kufanya mazoezi, mambo yazidi kuwa rahisi.

**Mfano: Kufunza Washiriki Kujishughulisha Ulimwenguni**

Kote ulimwenguni, watu wanowekelea maanani mahala pa makumbusho ili kuafikiana na yale yaliyopita ili waweze kupanga yale yajayo. Kutoka kwa makumbusho ya kibinafsi, kufikia makumbusho kirasmi, Watu hukusanyika mahala za makumbusho wakitafuta uganguzi, maelewano na njia za kusonga mbele. Ukumbusho ni lugha muhimu ya wanaharakati wa kupigania haki za binadamu. Hapo ndipo ukiukaji wa haki za binadamu unaonekana na kujulikana, mambo hujadiliwa na mbinu za kuzuiza ukiukaji zakuzwa. Kwa ufupi hizi mahala zaweza kuwa chombo maalum cha kukuza desturi za haki za kibinadamu.
Muungano wa Kimataifa wa Mahala za Dhamira (International Coalition of Sites of Conscience) ni mtandao wa kimataifa wa mahala za kihistoria ambao unatumia nguvu za hizi mahala kufundisha umma jinsi ya kujishughulisha na mambo ya haki za binadamu. Kwa mfano, mshiriki mmoja Memoria Abieta anapanga kufungua Nyumba ya Ukumbusho kwenye jumba moja ambayo ilitumiwa kutesa watu ili wananchi "wakumbuke kuazima kusuluhisha matatizo ya nchi yetu."

**6: Mbinu ni Njia ya Kufundisha**

Mbinu ni njia ya kushughulisha washiriki na waandani kwenye kazi ya kikundi. Mbinu zingine zaweza kuwa za mda mfupi na zingine za mda mrefu. Lakini zote pamoja zahitaji mpango, uratibu na mwelekeo. Zinawapa wananchi fursa ya kushiriki, kujifunza na kuazimika kwa kazi au kampeni ya kikundi. Kushiriki kutumia mbinu ni funzo muhimu kwa wafanyikazi wapya na wafanyi kazi wanaojitolea.

**Mfano: Mbinu kwa mafundisho**.

Kituo cha Walioteswa (*Centre for Victims of Torture,CVT*), kilichoanzisha mradi wa mbinu mpya kimeanzisha mkondo wa mazoezi kamambe na usimamizi ya wakimbizi ya kukuza uwezo wa umma na pia kuleta maelewano na ujuzi wa afya ya bongo ili kujenga jamii baada ya ukatili na ukiukaji wa haki za binadamu . CVT imeenzisha mafunzo kwenye kambi za wakimbizi kule Guinea na Sierra Leone. Haya mafunzo inatumia uwezo na usimamizi tawilishi wa hawa wakimbizi. Hawa wakimbizi majuzi wa afya ya akili wameweza kujipatia ujuzi, na pia kusaidia wengine ambao wanastahimili ili kusaidia kujenga jamii yao. Wakati huu, kuna wajuzi wa afya ya akili 122 wanaoshiriki katika huu mradi pamoja na wakimbizi maelfu ambao wanapata huduma tofauti tofauti.

**Uhaji wa kubuni mbinu mpya**

Kubuni mbinu mpya ni muhimu kwa kutekeleza haki za binadamu ulimwenguni. Tukipanua mafikira yetu kimkakati au kimbinu, jamii ya wanaopigania haki za binadamu wapata fursa ya kufanikiwa. Kwa ufupi:

- Mbinu chache yatupa maeneo machache. Mbinu kadha yatupa au yashirikisha maeneo makubwa.
- Kurudia mbinu moja wakati wote yaelekeza utumiaji wakati usiofaa. Mafikira ya mbinu nyumbufu yatupa fursa ya kuathiri shabaha yetu vyema.
- Mbinu iliyotumika mara kwa mara yahimiza wapinzani wetu kujitetea vyema. Unyumbufu wa mbinu unamudu mafunzo na pia miujiza.